

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

---

TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE  
YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI  
CHA KUENZIA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

---

Idara ya Kamati za Bunge,  
Ofisi ya Bunge  
S.L.P. 941  
**DODODMA**

04 FEBRUARI, 2020

# YALIYOMO

YALIYOMO .....	i
SEHEMU YA KWANZA .....	1
1.0 UTANGULIZI .....	1
1.1 Majukumu .....	1
1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu .....	1
1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati.....	2
1.3.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2018/2019.....	2
1.3.2 Kuchambua Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 .....	3
1.3.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais.....	3
1.3.4 Kushiriki katika Semina za Ndani .....	3
1.3.5 Ziara za Ukaguzi wa Shughuli za Ofisi ya Rais.....	4
SEHEMU YA PILI .....	5
2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI.....	5
2.1 Maelezo ya Jumla .....	5
2.1.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) .....	5
2.1.2 Ofisi ya Rais, Menejimet ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ..	5
2.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo .....	6
2.2.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais .....	15
2.2.3 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa .....	16
2.2.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora .	24
2.2.5 Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji .....	30
2.2.6 Semina kwa Wajumbe wa Kamati.....	43
2.2.7 Ziara za Ukaguzi wa Miradi.....	45
2.2.8 Muswada wa Sheria.....	46
SEHEMU YA TATU.....	48
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO.....	48
3.1 Maoni .....	48
3.2 Mapendekezo.....	51
3.2.1 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).....	51
3.2.2 Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari.....	51
3.2.2.1 Matumizi ya Force Account.....	51
3.2.2.2 <i>Utamaduni wa kufanya ukarabati wa mara kwa mara</i> .....	52
3.2.3 Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities	
3.2.4 Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART).....	53
3.2.7 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).....	55
3.2.8 Usalama wa Serikali Mtandao .....	56
3.2.9 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).....	56
SEHEMU YA NNE .....	59
4.0 HITIMISHO.....	59

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Taarifa hii inaelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitimiza majukumu ya kikanuni ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

### 1.1 Majukumu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inasimamia shughuli za Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kinaeleza kuwa majukumu ya Kamati hii yatakuwa: -

- a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

### 1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

- a) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais ili kufahamu Muundo na Majukumu na shughuli zinazotekelezwa;
- b) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais;
- c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari,2016; na
- d) Mafunzo na Semina za kuwajengea uwezo (*capacity building*) Wajumbe wa Kamati.

Lengo la kutumia mbinu hizo tofauti ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kina kuhusu nyanja ambazo wamepewa wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

### **1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia ipasavyo masharti ya kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

#### **1.3.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Miradi iliyohusika ni ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 na inatekelezwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kama ifuatavyo: -

##### **i) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP);
- Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA); na
- Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Vijana Wenye Ulemavu (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri)

ii) **Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala**

- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); na
- Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

**1.3.2 Kuchambua Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, katika kutekeleza jukumu la kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi huo ulilenga kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**1.3.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, ili kutekeleza jukumu la kikanuni ambalo chimbuko lake ni katiba [(Ibara ya 63 (2)], la kuisimamia na kuishauri Serikalila. Hoja mbalimbali ziliibuliwa kutokana na mijadala ya taarifa hizo na ufafanuzi wake unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

**1.3.4 Kushiriki katika Semina za Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati ya Utawala walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge (Legislative Support Programme), Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais (TASAF, Uongozi Institute, Wakala wa Serikali Mtandao – eGA) pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Kamati. Miongoni mwa taasisi hizo ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto – UNICEF, Wadau wa Kituo cha Kudhibiti na

Kupambana na Magonjwa – CDC kutoka Chuo Kikuu cha Maryland Baltimore cha nchini Marekani.

Lengo la Semina hizo lilikuwa kuwaongezea uelewa Wajumbe wa Kamati katika nyanja mbalimbali pamoja na kuwakumbusha kuhusu wajibu na majukumu ya Kibunge ambayo wanayatekeleza katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

### **1.3.5 Ziara za Ukaguzi wa Shughuli za Ofisi ya Rais**

**Mhehimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Rais, kupitia Taasisi na Idara zake. Msingi wa ziara hizi ni kuwapa Wajumbe wa Kamati fursa ya kujiridhisha kuhusiana na utekelezaji uliofanyika katika maeneo mbalimbali ambayo Taarifa zake ziliwasilishwa na Serikali kwenye Kamati kabla ya ziara hizo.

### **1.3.6 Uchambuzi wa Muswada wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipewa jukumu la kuchambua Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019 (The e- Government Authority Act, 2019) ambao ulilenga kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

#### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya taarifa inaelezea kwa ufasaha majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika kwa kuanisha Wizara, Taasisi na Idara iliyohusika na kuonesha mafanikio na changamoto. Aidha, ili kufafanua zaidi na kuongeza uelewa katika baadhi ya maeneo ya uchambuzi wa matokeo, sehemu hii itatumia takwimu na **vielelezo/michoro**.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ilikutana na kutembelea Ofisi ya Rais kama ifuatavyo: -

##### 2.1.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

- a) Mikoa Ishirini na Sita (26) ya Tanzania Bara;
- b) Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA);
- c) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART);
- d) Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) – Hombolo;
- e) Shirika la Masoko Kariakoo (KMC); na
- f) Shirika la Elimu Kibaha (KEC).

##### 2.1.2 Ofisi ya Rais, Menejimet ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

- a) Wakala wa Serikali Mtandao (eGA)
- b) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- c) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC);
- d) Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA);
- e) Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- f) Wakala wa Ndege za Serikali; na
- g) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayochambuliwa katika sehemu hii kuhusu Wizara, Taasisi na Idara zilizoanishwa hapo juu yamegawanyika kama maeneo yafuatavyo: -

- a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

- b) Uchambuzi wa Bajeti;
- c) Taarifa za Utekelezaji;
- d) Ziara za ukaguzi wa shughuli za kiutendaji; na
- e) Uchambuzi wa Miswada.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

### 2.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotengewa na kuidhinishiwa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo inatekelezwa na Ofisi ya Rais, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Ukaguzi huo ulilenga kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na thamani halisi ya fedha "*value for money*" iliyotolewa. Aidha, Wajumbe wangeongeza uelewa na hivyo kuishauri vyema Serikali wakati wa uchambuzi wa bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata. Ifuatayo ni baadhi ya miradi iliyokaguliwa na Kamati: -

#### a) Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kupitia Kifungu 1009 "*Infrastructure Development Division*" chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mradi huu unagharamiwa na mkopo kutoka Benki ya Dunia na ruzuku kutoka Serikali ya Denmark tangu mwaka wa fedha 2010/2011 na utaendelea hadi mwaka 2020/2021 kwa thamani ya **Dola za Marekani milioni 355.7.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ambako unaotekelezwa chini ya Kifungu 8091, Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara.

Mradi unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za miji na uimarishaji wa mifumo ya Halmashauri katika kutoa huduma bora kwa jamii. Barabara zenye urefu wa kilomita 15.78 zimejengwa



kwa kiwango cha lami kwa jumla ya **shilingi bilioni 24.01**. Barabara hizo ni Bandari (kilomita 2.75), Zambia (kilomita 3.75), Mikindani (kilomita 1.9), Chuno (kilomita 5.78) na Kunambi (kilomita 1.6).

Aidha, ujenzi wa dampo la kisasa na vizimba 25 vya kukusanyia taka, pamoja na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kusafirishia taka kutoka kwenye vizimba hadi dampo viligharimu jumla ya **shilingi bilioni 4.96**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufanisi katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi hiyo, Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata nyongeza ya **shilingi bilioni 8.8** ili kujenga mifereji ya maji yenye urefu wa kilimita 7.4 maegesho ya magari katika dampo, mizani ya kupimia taka na uwekaji wa taa za nishati ya jua katika barabara ya Chuno.

Aidha, **shilingi bilioni 21.68** zitatumika kujenga barabara (kilomita 4.1), mfereje wa kupeleka maji baharini (kilomita 3.4), kuboresha maeneo ya wazi, maduka makubwa, stendi ya daladala ya Mikindani, ujenzi wa soko la kisasa la Chuno, kazi zitakazotekelezwa na Mkandarasi M/s Jiangxi Geo Engineering Group kutoka China.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania umekuwa na faida nyingi ikiwa ni pamoja na; kuongeza kilomita 18.8 za mtandao wa barabara za lami, kukuza uchumi kwani taa za barabarani zimewezesha wananchi kufanya biashara nyakati za usiku; kuboresha usafi wa mji kwa kuzoa taka na kuzipeleka dampo la kisasa na hivyo kusaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na mengineyo.

Licha ya mafanikio yaliyoshuhudiwa na kamati, zipo changamoto kadhaa ambazo zinaweza kuzorotesha utekelezaji wa mpango huu. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa stendi ya daladala ya Mikindani kutokana na kutokamilika kwa

zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliohama ili kupisha mradi, na kasi ndogo ya ujenzi wa barabara kutokana na msimu wa mvua.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inakamilisha zoezi la fidia kwa haraka ili wananchi wanaohusika waweze kupisha ujenzi uendeleo kwa haraka.

#### **b). Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, wakala huu ambao ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 ulianza kuteleleza majukumu yake mwaka 2017 na unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 108,946 nchi nzima. TARURA inafanya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini pamoja na madaraja ili kuwezesha barabara kupitika muda wote. Inatarajiwa kuwa utendaji wa TARURA utachangia kuinua shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuboresha barabara katika maeneo muhimu ya viwanda, machimbo ya madini na kilimo.

Ili kujiridisha na utekelezaji wa shughuli za TARURA Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mkoani Lindi ambapo Wakala inahudumia barabara zenye urefu wa kilomita 693.1. Kamati ilikagua barabara ya Nyengendi (1km) inayojengwa kwa kiwango cha lami ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyengendi - Mnara-Rutamba yenye urefu wa kilomita 48, na kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi - Nyangao Hospital (0.8 km) ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyangao - Namupa-Mihima yenye urefu wa kilomita 23.2

Ujenzi wa barabara hizo unatekelezwa na Nyumbani Construction Company Ltd kwa gharama ya **shilingi milioni 531.93** na umefikia wastani wa asilimia 38.5. Kukamilika kwa kipande cha barabara ya Nyengendi - Mnara - Rutamba kutarahisisha huduma za usafiri kutoka barabara kuu ya Lindi - Mtwara kwenda eneo la Rondo

ambako kuna Msitu wa Hifadhi ya Taifa na hivyo kuchochea shughuli za utalii.

Aidha, kukamilika kwa kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi – Nyangao Hospitali kutarahisisha usafiri kwa wakazi wa kata ya Nyangao na Namupa, kutoka barabara kuu ya Lindi - Masasi kwenda Hospitali teule ya wilaya (Nyangao - DDH) kupata huduma za matibabu

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa shughuli za TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi umesaidia kuboresha huduma ya usafiri kwa wananchi kutoka barabara kuu ya Lindi - Masasi kwenda katika Hospitali Teule ya Wilaya (Nyangao DDH). Aidha, kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutaongeza thamani ya ardhi katika kata sita ambazo maeneo yake yako jirani na barabara hizo.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ya matengenezo ya barabara ikilinganishwa na mahitaji halisi, ukosefu wa usafiri wa uhakika wa kuwezesha kuafuatilia na kusimamia ujenzi wa barabara na upungufu wa Wataalam wa ujenzi (wahandisi).

Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya TARURA na kuajiri Wataalam wa ujenzi wanaohitajika katika Halmashauri ya Lindi ili kuwezesha utekelezaji na usimamizi thabiti wa miradi ya miundombinu ya barabara inayotekelezwa na TARURA).

- (c) **Mradi Na.4946 – Local Government Authority Own Source Projects ‘Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu’**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya **shilingi bilioni 3.01** na kutekelezwa chini ya Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara. Kupitia mradi huu Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu

huwezesha kiuchumi kwa kupatiwa mafunzo na mitaji kutokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini. Hadi Desemba, 2018 jumla ya Vikundi 1,213 kutoka makundi hayo, vilikuwa vimenufaika na kiasi hicho cha fedha kilichotengwa.

Kamati ilitembelea Vikundi vitatu ambavyo ni kikundi cha Wanawake cha Tunalekane; kikundi cha Vijana cha Tuvamo na kikundi cha wenye Ulemavu cha Wajibu.

**i. Kikundi cha Wanawake cha Tunalekane (Tunalekane Women Group)**

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki chenye wanachama watano (5) kilianzishwa mwaka 2012 na kinajishughulisha na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa sabuni za maji na vipande, mafuta ya mgando na batiki kwa wajasiriamali wengine. Aidha, kinafuga kuku, kupika vyakula kwenye sherehe na kuuza vifaa vya utengenezaji wa sabuni na batiki.

Tangu kuanzishwa kikundi hiki kimeishapata mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 12** kwa awamu tatu na kupokea mafunzo ya ujasiriamali kutoka Manispaa ya Mtwara Mikindani, ambavyo vimewezesha wanakikundi kujikwamua kiuchumi wao pamoja na familia zao. Aidha, kikundi kimeweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali zaidi ya 670 katika mikoa ya Mbeya na Mtwara.

Kupitia kipato wanachopata, wanakikundi hao wamemudu kusomesha watoto, kupata mahitaji ya nyumbani na pia mtaji kwa kila mwanachama ili kuendesha shughuli za kiuchumi nje ya kikundi.

## ii. Kikundi cha Vijana cha Tuvamo (Tuvamo Group)

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2016 na vijana watano (5) wa kiume walioamua kuanzisha shughuli ya kutengeneza na kuuza samani, kukarabati majengo (upauaji, kufunga jypsum) na kukopeshana fedha kwa hiyari.

Kikundi kilianza kwa mtaji wa **shilingi milioni 2** na hadi Kamati inafanya ziara mtaji ulikuwa umefikia **shilingi milioni 14** baada ya kupata mkopo mwaka 2018 kupitia Mfuko wa kuwezesha kiuchumi, Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu.

Kupitia miradi hii kikundi kimeweza kutoa ajira kwa vijana wanne (4) ambao ni mafundi; kuongeza uzalishaji wa samani na hivyo kukuza kipato cha kila mwanakikundi sambamba na kuchangia mapato ya Serikali kwa kulipa kodi.

## iii. Kikundi cha Watu wenye Ulemavu cha Wajibu (Wajibu Disabled Group)

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki ambacho kinaundwa na watu wenye ulemavu watano (5) wanaume watatu na wanawake wawili, kilianzishwa mwaka 2018 ili kujishughulisha na uchomeleaji (welding), ushonaji (tailoring) na biashara ndogondogo sokoni.

Kikundi kilianza shughuli zake na mtaji wa **shilingi milioni 4.7** uliotokana na mkopo usio na riba kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani. Kamati ilipotembelea kikundi hicho tayari kilikuwa kimerejesha asilimia 12 ya mkopo huo na kimejipanga kurejesha fedha yote ndani ya wakati uliopangwa.

Shughuli za kikundi zimewezesha wanachama wake kujimudu kiuchumi kwa kupata mahitaji muhimu ya chakula, matibabu,

mavazi na kusaidia kuondoa hali ya unyanyapaa kwa wanachama kutokana na Ulemavu walio nao.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia ukaguzi wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani Kamati ilibaini mafanikio na changamoto kadhaa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ajira kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambao ni wanachama wa vikundi vilivyotembelewa, na ongezeko la mapato ya manispaa kutokana na ulipaji wa kodi stahiki.

Aidha, kumekuwa changamoto za kukosa soko la uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa na vikundi kama vile samani, na batiki, na kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali. Kamati imeshauri Serikali kutumia Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kabla ya kuwapatia mikopo ya kuanzisha shughuli za kiuchumi.

d) **Mradi Na. 4921 – Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, mpango huu unatekelezwa chini ya kifungu 1003 *“Policy and Planning”* cha fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. MKURABITA inaandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika kisheria ambao huwezesha wananchi wanyonge kurasimisha ardhi na biashara wanazomiliki.

Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri ya Nachingwea na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Mbondo, Nahimba na Nakalonji ambako jumla ya mashamba 2,328 yameweza kupimwa na Hati za Haki miliki za kimila 1,341 kuandaliwa.

Aidha, MKURABITA imewezesha vijiji 104 kati ya 127 katika halmashauri hiyo kupima mipaka yake na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa mafanikio yaliyobainika kutokana na zoezi la urasimishaji ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi na mipaka ya miliki katika vijiji husika; Wanawake kupata fursa ya ama kumiliki Hati za haki miliki ya ardhi peke yao au kwa kushirikiana na wenza wao; na maeneo kuongezeka thamani kwa ardhi ya wananchi katika maeneneo yaliyorasimishwa.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti na ukosefu wa wataalamu wa kuandaa na kusajili Hati za haki Miliki za Kimila, jambo linaloathiri kasi ya urasimishaji wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutatua changamoto hizo Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya MKURABITA na wataalamu wa kuandaa na kusajili hati za haki miliki za kimila ili kuwezesha zoezi la urasimishaji katika maeneo mengine ya Halmashauri ya Nachingwea.

e) **Mradi Na.6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF) – Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa **shilingi bilioni 74.36** na ulipangwa kutekelezwa chini ya kifungu 1003 *“administration and human resource management”* cha Fungu 30 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. TASAF inatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, na uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji ambayo inasaidia kaya maskini kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato. Hadi sasa takribani kaya maskini zaidi ya **milioni 1** zenye jumla ya Watanzania **milioni 5** zimeandikishwa kunufaika na mpango.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango huu, Kamati ilitembelea Kijiji cha Namela kilichopo katika Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara ambacho ni miongoni mwa vijiji 99 vinavyonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini katika wilaya hiyo. Kijiji hiki kina jumla ya Kaya 117 zinazonufaika na mpango huu ambazo zilikuwa zimepokea ruzuku ya **shilingi milioni 109.99** kutokana na awamu 30 za uhawilishaji tangu kuanza kwa mpango huo Julai – Agosti,2014 hadi Januari – Februari,2019.

Aidha, TASAF imewezesha kijiji cha Namela kutekeleza miradi ya utoaji wa ajira za muda kwa kaya zote 117 za walengwa kwa kugharamia mradi wa upandaji wa mikoko katika eneo la ufukwe wa bahari ya Hindi lenye ukubwa wa ekari 4 kwa gharama ya **shilingi milioni 14.46** na ujenzi wa kisima cha pete kwa gharama ya **shilingi milioni 14.89**. Jumla ya **shilingi milioni 7.12** zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mahudhurio ya watoto shuleni hasa wanaotoka katika kaya za walengwa tofauti na awali; walengwa wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, ufugaji, kilimo, na biashara na hivyo kuboresha maisha ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wananchi kukosa uelewa kuhusu utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini jambo ambalo limeibua malalamiko kutoka kwa kaya ambazo hazijaingizwa kwenye mpango.

Kamati ilishauri Serikali kuwajengea uelewa wa kutosha wananchi kuhusu utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, pamoja na kuhakikisha kaya zenye sifa zinaingizwa kwenye mpango.



f) **Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, chuo kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali, Agosti, 2000 kwa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili, Chuo cha Watumishi wa Serikali (Civil Service Training Centre) kilichokuwa Dar es Salaam na Chuo cha Uhazili Tabora (Tabora Secretarial College). Uanzishwaji wa chuo hiki ulilenga kusaidia maboresho katika Utumishi wa Umma ili kuleta tija katika utoaji wa huduma.

Tangu kuanzishwa kwake chuo kimeweza kuongeza matawi hadi kufikia sita ambayo ni Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Mbeya, Tabora na Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Mtwara na kubaini mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa wahitimu 8,560 katika fani mbalimbali tangu mwaka 2009, kupata usajili kamili kutoka Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE), kumiliki viwanja viwili katika eneo la Shangani na kupunguza watumishi wa mikataba kutoka asilimia 76 hadi asilimia 41.

Pamoja hayo mafanikio hayo bado kuna changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na uhaba wa mabweni jambo linalozuia ongezeko la udahili wa wanafunzi, upungufu wa vitabu 200 na uchakavu wa majengo ambao unahatarisha usalama wa watumiaji.

Kamati imeshauri Serikali kujenga Mabweni ya kutosha ili kuongeza udahili wa wanafunzi na kukarabati majengo yaliyochakaa ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza iwapo uchakavu utaachwa kuendelea.

2.2.2 **Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha zoezi la ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilijielekeza katika uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais ili kuzingatia Kanuni ya 98 (2), pamoja na kifungu cha 7(1) cha

Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Bajeti ya Ofisi ya Rais inahusisha Mafungu 28 kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mafungu 8 kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Uchambuzi ulijikita katika kupitia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti vilifanyika kama ifuatavyo: -

### 2.2.3 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti katika Ofisi hii ulihusisha mafungu yafuatayo: -

- 1) Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI
- 2) Fungu 2 - Tume ya Utumishi wa Waalimu (TSC)
- 3) Fungu 70 – Mkoa wa Arusha
- 4) Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya
- 5) Fungu 79 – Mkoa wa Morogoro
- 6) Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam
- 7) Fungu 63 – Mkoa wa Geita
- 8) Fungu 90 – Mkoa wa Songwe
- 9) Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa
- 10) Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara
- 11) Fungu 81- Mkoa wa Mwanza
- 12) Fungu 84 – Mkoa wa Singida
- 13) Fungu 85 – Mkoa wa Tabora
- 14) Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro
- 15) Fungu 71 – Mkoa wa Pwani
- 16) Fungu 36 – Mkoa wa Katavi
- 17) Fungu 73 – Mkoa wa Iringa
- 18) Fungu 87 – Mkoa wa Kagera
- 19) Fungu 54 – Mkoa wa Njombe
- 20) Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma
- 21) Fungu 76 – Mkoa wa Lindi
- 22) Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu
- 23) Fungu 95 – Mkoa wa Manyara
- 24) Fungu 77 – Mkoa wa Mara
- 25) Fungu 72- Mkoa wa Dodoma
- 26) Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma
- 27) Fungu 83 – Mkoa w Shinyanga

28)Fungu 86 – Mkoa wa Tanga

**Mheshimwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikani wa fedha za matumizi kutoka Hazina kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa

(i) **Ukusanyaji Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imekusanya **shilingi bilioni 9.85** sawa na asilimia 44 tu ya lengo la kukusanya **shilingi bilioni 22.64** katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Kamati ilielezwa kwamba makusanyo hafifu ya maduhuli yamechangiwa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) kushindwa kupata **shilingi bilioni 1.2** ilizotarajia kutoka Benki ya CRDB; baadhi ya halmashauri kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; na Mauzo hafifu ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na asilimia 43.7 iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Ingawa kiwango kilichokusanywa kiko chini ya asilimia 70 iliyopaswa kufikiwa hadi katika robo ya tatu, bado ni kikubwa kwani malengo yaliyowekwa yalikuwa makubwa zaidi ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Aidha, uchambuzi umebaini kwamba, makusanyo yamekuwa yakiongezeka katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha (2016/17, 2017/18 na 2018/19).

Kwa mtazamo wa Kamati ilikuwa vigumu kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kipindi kilichokuwa kimesalia, na hivyo kutishia kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 makusanyo yalikuwa ni **shilingi bilioni 735.73**, sawa na wastani wa asilimia 69, kiwango ambacho kinapaswa kuwa kimefikiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa bajeti. Bado Halmashauri ziimeendelea kuwa na makusanyo makubwa ikilinganishwa na mikoa na makao makuu (Fungu 56) na taasisi zake.

#### (ii) **Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa umebaini kwamba fedha zinazotolewa zimeendelea kupungua kwa mwaka wa tatu mfululizo; mwaka wa fedha 2016/17 (asilimia 57), mwaka wa fedha 2017/18 (asilimia 53) na mwaka wa fedha 2018/19 (asilimia 45.2).

Aidha, fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) uliowekwa; fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na fedha hazitolewi kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 181.73** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 45.2** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo huo unaonesha kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 53 iliyopatikana katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2019 ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 21.75** sawa na asilimia 50.6 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 18.4 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/18.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi bilioni 159.98** sawa na asilimia 44.5 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2018/19 ziliidhinishwa **shilingi trilioni 5.89** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 3.94** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi bilioni 580.2** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni **1.37** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 57, wakati fedha za maendeleo zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 38.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2018/19 ulikuwa ni **asilimia 47.55**,

kiwango ambacho kimepungua sana ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 60.5** katika miaka miwili ya fedha iliyopita (2016/17 na 2017/18).

Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, badala ya upatikanaji wa fedha kuongezeka ili kufikia lengo la angalau asilimia 25 kwa kila robo katika mwaka fedha, sasa wastani umeshuka hadi kufikia asilimia 15.85 kwa robo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa asilimia 47.5. Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hii inaashiria kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kusuasua kutokana na fedha kucheleweshwa na kutolewa kwa kiasi kidogo.

**(iii) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imezingatia maouni na ushauri wa Kamati kwa kiwango cha kuridhisha, jambo ambalo limesaidia kutatua changamoto zilizobainishwa, na hivyo kuboresha huduma za msingi kwa maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

- (a) Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria utakaowezesha kusimamia kikamilifu asilimia kumi (10) ya

mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Sheria hiyo ilitungwa kupitia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 iliyofanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 37 A, na sheria hiyo ilianza kutumika Julai, 2018;

- (b) Halmashauri ziendeele kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imebuni miradi ya kimkakati ili kuziwezesha Halmashauri kuongeza mapato ya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019 Halmashauri 30 zilikuwa zimekidhi vigezo vya miradi 38 ambayo iliidhinishiwa **shilingi bilioni 268.4**;

**Mheshimiwa Spika**, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na: -

- i. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu fedha za asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri na kuzipeleka kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Aidha, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na idadi ya vikundi vilivyopokea pesa, na kusimamia urejeshaji wa fedha hizo; na
- ii. Serikali iendeele kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma katika halmashauri nchini ambayo yalijengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Serikali iliidhinisha **shilingi trilioni 1.36** kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini hadi Desemba, 2018

ni asilimia 38 tu ya fedha hizo ndiyo ilikuwa imetolewa. Hii inaashiria kwamba, ukamilishaji wa miradi ikiwa ni pamoja na maboma utaendelea kusuasua.

**iv.) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoja na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 6.21**. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 4.52** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **shilingi trilioni 1.69** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida **shilingi trilioni 3.81** sawa na asilimia 61.33 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na **shilingi bilioni 707.95** sawa na asilimia 11.40 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo imechukua asilimia 27.27 ya bajeti yote ya Ofisi hii. **Jedwali Na. 01** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 01** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020

<b>Mgawanyo wa Bajeti</b>	<b>Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020</b>	<b>Asilimia ya Makadirio (%)</b>
OC	707,951,000,000	11.40
Mishahara	3,807,104,425,000	61.33
Maendeleo	1, 692, 937, 354,769	27.27
<b>Jumla</b>	<b>6, 207,992, 779,769</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2019/2020)



**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa makusanyo ilikadiriwa kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitakusanya jumla ya **Shilingi bilioni 802.16**. Mapato hayo yameongezeka kwa **shilingi bilioni 43.79** sawa na asilimia 6 ikilinganishwa na makusanyo ya **shilingi bilioni 758.36** katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Ongezeko hilo lilitarajiwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa takribani **shilingi bilioni 29.89** sawa na asilimia 4.1 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha uliomalizika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipongeza hatua za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kufidia pengo la vyanzo vilivyochukuliwa na Serikali Kuu, na kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, kwani kumekuwa na tija kubwa.

Kwa ujumla wake bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipungua kwa **shilingi bilioni 374.95** sawa na asilimia 5.69 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, Kamati ilibaini upungufu wa asilimia 5.92 kutoka **shilingi trilioni 1.79** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi **shilingi trilioni 1.69** katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Uchambuzi ulibaini kwamba, upungufu huo wa bajeti ya jumla na ile ya maendeleo ulitarajiwa kubadili kabisa mwelekeo wa bajeti kwa ofisi hii ambayo iliongezeka kwa wastani wa asilimia 9 katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2016/17 hadi 2018/19).

Aidha, katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 uchambuzi

ulibaini kwamba, wakati bajeti ya Taifa ikiongezeka kwa asilimia 1.93 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho ilipungua kwa asilimia 5.69.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na asilimia 18.74 ya bajeti ya Taifa, uwiano ambao uliendelea kupungua katika kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2015/16 ambapo uwiano ulikuwa ni asilimia 24.

**Mheshimiwa Spika**, inashangaza kwamba licha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kusimamia sekta nyingi katika ngazi za mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti yake imepungua, na uwiano wa bajeti hii ikilinganishwa na bajeti ya Taifa umeendelea kupungua kwa mwaka wa nne mfululizo.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iendelee kuimarisha mfumo wa kuwahudumia wananchi ambao ndiyo msingi wa madaraka yote ya Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977. Njia madhubuti ya kuimarisha mfumo huo ni kupeleka kikamilifu fedha za kutosha (kuongeza bajeti) kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika.

#### 2.2.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utawala Bora, Kamati ilifanya uchambuzi wa mafungu yafuatayo: -

1. Fungu 20 – Ikulu;
2. Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
3. Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
4. Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
5. Fungu 67 – Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa

Umma;

6. Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma;
7. Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; na
8. Fungu 04 – Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

#### (i) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi kilichotolewa na Hazina. Aidha, mtiririko wa fedha haukuwa mzuri kwani fedha ilikuwa inatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) ulioandaliwa.

Uchambuzi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi bilioni 374.7**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 60.03 ya Fedha yote iliyoidhinishwa.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa Fedha kwa mwaka 2018/2019 na mwaka 2017/2018 na kubaini kuwa kiasi hicho cha fedha kilipungua kwa takribani **shilingi bilioni 43** sawa na asilimia 10.31 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho kilikuwa ni **shilingi bilioni 417.7**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 ofisi hii na Mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 82.05** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 46.87** ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kilipungua kwa asilimia 60.19 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho kilikuwa ni **shilingi bilioni 206.72**.

Kamati imebaini kwamba, ingawa mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukufikia lengo linalohitajika, ulimarika ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliotangulia. Kwa wastani upatikanaji wa fedha ulikuwa ni asilimia 65.03 ya fedha zote zilizoidhinishwa, wakati katika mwaka uliotangulia ilikuwa ni asilimia 50.37. Aidha, kasumba ya

fedha za matumizi ya kawaida kupatikana kwa wingi kuliko fedha za maendeleo imeendelea kutamalaki.

**(ii) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilizingatia kikamilifu baadhi ya maoni ya Kamati, na ilikuwa inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu: -

- (a) Serikali kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi ambapo iliweza kuidhinisha asilimia 81 ya nafasi za uteuzi;
- (b) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu (Sheria, Kanuni na Miongozo) na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima. Mafunzo yalitolewa kwa wakurugenzi wa serikali za mitaa, wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na wilaya; na
- (c) Benki na Taasisi za fedha zielimishwe kuhusu hadhi ya Hati za Haki Miliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, ambapo baadhi ya benki na taasisi za fedha zimeanza kukubali hati hizo baada ya kuelimishwa. Aidha, wananchi zaidi ya 500 wametumia hati hizo kukopa **shilingi bilioni 4.9** kutoka Benki za CRDB, NMB, PSPF na Agricultural Inputs Trust Fund; na
- (d) Kutambua na kuandikisha Kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji

wa TASAF III yako katika hatua za mwisho na maeneo yote hayo yatafikiwa.

(iii) **Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, ili iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iliomba kuidhinishwa jumla ya **shilingi bilioni 683.51**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 483.66** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi bilioni 199.87** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, bajeti iliyoombwa kuidhinishwa katika mwaka huu iliongezeka kwa **shilingi bilioni 14.43** sawa na asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilikuwa **shilingi bilioni 669.09**. Ongezeko hilo la fedha lilibadili mwenendo wa bajeti ya ofisi hii kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19) ambapo bajeti ilikuwa ikipungua.


Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi ulibaini ongezeko la **shilingi bilioni 3.89** sawa na asilimia 1.99 ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi bilioni 195.97** zilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19. Uchambuzi zaidi ulibaini kwamba licha ya ongezeko hilo, bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu ilikuwa ni takribani asilimia 51.12 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi ulilengwa kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti

ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-


- (a) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni **shilingi bilioni 683** ni sawa na asilimia 2.06 tu ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2019/20 ni **shilingi trilioni 33.1**
- (b) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ulionyesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 1.93, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/19; ilihali bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilionezeka kwa asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19;
- (c) Mpango wa Maendeleo ya Taifa ulionyesha ongezeko la asilimia 2.0 katika fedha za maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2019/20, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, iliongezeka kwa asilimia 1.99 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-

Figure 1 Chati Na. 01: Bajeti ya Taifa kwa ajili ya mishahara, Matumizi ya Kawaida, Maendeleo na Deni la Taifa kwa Mwaka 2019/20



**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20

Figure 2 Chati Na. 02: Bajeti ya OR-UUB kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo kwa Mwaka 2019/20



**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa fedha 2019/2020

### 2.2.5 Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 7 (1) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Taarifa hii itahusisha uchambuzi wa taarifa za utekeleza za baadhi ya taasisi.

(a) **Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali Nchini**

**Mheshimwa Spika,** mkakati huu unalenga kurejesha shule kongwe katika ubora wake baada ya miundombinu yake kuchakaa na kuharibika kwa kiwango kikubwa. Mkakati huu



ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na unagharamiwa na Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Program For Results – EPSR).

Jumla ya shule 89 kongwe zitakarabatiwa kwa awamu kwa kuhusisha vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, ofisi za walimu, majiko, mifumo ya maji safi na taka, mifumo ya umeme na TEHAMA. Awamu ya kwanza yenye shule 45 utekelezaji wake ulianza mwaka wa fedha 2016/2017 na kugharimu **shilingi bilioni 54.85**.

Aidha, utekelezaji wa awamu ya pili yenye shule 19 ulianza Mei, 2019 kwa gharama ya **shilingi bilioni 16.85** ambapo utaratibu wa *force account* unatumika na ukarabati uko katika hatua mbalimbali. Vilevile, maandalizi kwa ajili ya ukarabati kwa shule zilizosalia yameanza kufanyika kwa hatua za upembuzi yakinifu (*conditional survey*) na inakadiriwa kwamba, utagharimu **shilingi bilioni 16.46**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuzikarabati shule kongwe nchini kwa lengo la kurejesha ubora wa awali ambao pia unaleta mazingira bora ya kazi kwa walimu na ya kujifunzia kwa wanafunzi. Jambo hili linarejesha heshima ya shule za Serikali na kuongeza ari ya utendaji kwa Walimu.

Aidha, Kamati inapongeza hatua ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuanza mchakato wa kuacha na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika ukarabati wa baadhi ya shule kwani ameshindwa kuzingatia kikamilifu masharti ya mikataba aliyosaini ili kutekeleza ujenzi au ukarabati.

Vilevile, Kamati inashauri Serikali kujenga mazingira ya kukarabati shule hizo mara kwa mara, na kutunga sheria ndogo ndogo zitasaidia kulinda mazingira na miundombinu ya shule hizo ili kuepusha uharibifu na uchakavu kutokea bila kushughulikiwa.

(b) **Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unagharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na fedha za ruzuku kutoka Serikali ya Denmark na utekelezaji wake uko katika awamu ya

pili baada ya awamu ya kwanza iliyotekelezwa kwa miaka miaka mitano (2010/2011 hadi 2015/2016). Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Majiji Tano na Halmashauri za Manispaa tatu za Mtwara/ Mikindani, Kigoma/Ujiji Kigoma na Ilemela, na utagharimu jumla ya **dola za marekani milioni 355.7**.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikiwa miongoni mwa wanufaika wa mradi huu imeweza kujenga barabara za lami yenye urefu wa kilometa 42.29, Dampo la kisasa (Landfill) katika kijiji cha Chidaya, ununuzi wa makontena 61 ya kubeba taka ngumu, mfereji mkubwa wa maji ya mvua (storm water Drain) wenye urefu wa kilometa 7.64 na ukarabati wa Ofisi ya Mhandisi na ukarabati wa karakana ya Jiji. Kazi zote zilitekelezwa kwa gharama ya **shilingi bilioni 47.47**

**Mheshimiwa Spika**, ufanisi wa utekelezaji wa mradi huu umewezesha Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupata nyongeza ya mkopo mara mbili (first and second additional financing) ya **shilingi bilioni 88.8** ambazo zimetumika kukamilisha kazi za awamu ya kwanza, na pia kujenga barabara za lami kilometa 26.7, stendi ya mabasi ya kisasa, Soko la Kisasa la Job Ndugai, eneo la mapumziko (recreational park) la Chinangali, kituo cha maegesho ya malori Nala, na uwekaji wa taa za barabarani 925 zinazotumia umeme wa jua (solar street lights), ambapo ujenzi umefikia asilimia 82.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia TSCP kuboresha Jiji la Dodoma kwa ujenzi wa miundombinu hiyo ambayo ni mwanzo mzuri wa kulifanya jiji hili kuwa la kisasa, na kuwezesha wananchi kupata huduma bora za kijamii na kiuchumi.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ihakikishe Halmashauri ya Jiji la Dodoma inatafuta waendeshaji wenye sifa katika Stendi ya Mabasi, Soko, Kituo cha Mapumziko cha Chinangali, na Kituo cha kuegesha Malori cha Nala, ili kuhakikisha thamani ya pesa zilizotumika katika uwekezaji huo inapatikana.

Aidha, nitumie fursa hii kukupongeza Mheshimiwa Spika, kwa heshima uliyopewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, ya Soko jipya la Dodoma kuitwa kwa jina lako. Hii ni heshima kubwa, ambayo itafanya mchango wako katika Bunge la Tanzania na Mkoa wa Dodoma ikumbukwe katika historia ya nchi yetu.

**(c) Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, taasisi imeendelea na kusimamia malengo ya kuwa kituo cha utaalum wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika ikianza na Tanzania, Ukanda wa Mashariki na hatimaye Bara lote la Afrika. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

Taasisi hii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichopo Helsinki, Finland imeendelea kutekeleza Programu ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi ambayo inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati na kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine.

Tangu kuanza kwa mafunzo hayo, Watumishi waandamizi 33 kutoka Wizarani, Taasisi na Mashirika ya Umma wameweza kushiriki na ambapo wamepata ujuzi wa masuala ya Uongozi wa matokeo, ubunifu na kuandaa Mpango Mkakati na namna ya kuutekeleza.

Aidha, taasisi imeendesha kozi mbili (2) kwa Viongozi Waandamizi 36 kutoka Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu masuala ya uongozi, uongozi binafsi na akili hisia kwa lengo la kuimarisha utendaji wao.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi iliandaa na kuendesha vipindi vitano (5) vya majadiliano na Marais Wastaafu, Mheshimiwa Benjamini William Mkapu, Rais wa Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania; Mheshimiwa Ernest Bai Koroma wa Sierra Leone; Mheshimiwa Hery Rajaonarimampianina wa Madagasca; na Viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu kupitia runinga, tovuti ya Taasisi ya Uongozi na mitandao ya kijamii. Msingi wa vipindi hicho ambavyo vilirushwa kote barani Afrika ilikuwa kubailishana taarifa, maarifa na uzoefu wa kiuongozi.

Aidha, taasisi ya Uongozi imekuwa ikishirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa ya UNU-WIDER iliyopo Finland kufanya tafiti kuhusu uchumi wa viwanda, uchumi mpana, fedha, usimamizi wa mikopo endelevu pamoja na maeneo mengine, ambapo hadi sasa wamekamilisha tafiti 13.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hii imeweza kuandika na kuchapisha kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamini William Mkapu ambacho kilizinduliwa mwaka jana, na inaendelea na maandalizi ya kitabu kwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi huku ikiendelea kuhamasisha viongozi wengine wastaafu kuandaa na kuchapisha vitabu kwa kushirikiana na taasisi hii.

Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu ikiwezekana wa kisheria ambao utawataka viongozi wa ngazi ya uandamizi kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na taasisi hii kwa lengo la kujengewa uwezo au kuongezewa weledi katika masuala ya kiuongozi kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

**(d) Wakala wa Ndege za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Ndege za Serikali ilianzishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245. Awali ilikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi na ilipohamishiwa Ofisi ya Rais, tangu tarehe Aprili, 2018.

Pamoja na kusimamia huduma za usafiri wa ndege kwa viongozi wakuu wa kitaifa, Wakala unaratibu ununuzi wa ndege mpya za Serikali na kuzikodisha kwa kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili ziweze kutumika kibiashara. Hadi sasa Wakala inamiliki ndege 10 ambazo zimegawanyika katika makundi mawili (2), ndege nne (4) ambazo zinatumiwa kwa safari za Viongozi wakuu wa kitaifa na ndege sita (6) ambazo zimezokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Aidha, wakala imeweza kuwapeleka mafunzoni wanahewa 19 kwa ajili ya kupata mafunzo ya kisheria kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu zinazoratibiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ili waweze kuhuisha leseni zao.

Kamati inapongeza mafanikio ambayo Wakala imeyapata katika kipindi hiki cha awamu ya tano hasa kwa kununua ndege na kuzikodisha kwa Kampuni ya ATCL, jambo ambalo limewezesha shirika hilo kurejea angani na hivyo kuitangaza nchi yetu kimataifa.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ijenge utamaduni wa kulipa madeni yanayotokana na kukodisha ndege ili kuiwezesha Wakala kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi na hivyo kutoa huduma bora.

**(e) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, tangu ulipoanzishwa mwaka 2000 mfuko huu umetekelezwa katika awamu tatu tofauti. Katika awamu ya kwanza (2000 – 2005) iliyohusisha maeneo 42 (halmashauri za Tanzania Bara, na Unguja na Pemba) jumla ya **shilingi bilioni 72** zilitumiwa kuwahudumia

wananchi kupitia miradi mbalimbali ya afya, maji, miundombinu na elimu.

Kutokana na mafanikio yaliyopatikana, Serikali iliamua kuanzisha huduma za mfuko huo katika halmashauri zote 124 za wakati huo Tanzania Bara, pamoja na Unguja na Pemba kwa kuanzisha awamu ya pili (TASAF II) iliyotekelezwa kuanzia mwaka 2005 hadi 2013 kwa gharama ya **shilingi bilioni 430**.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kutekelezwa kwa TASAF Awamu ya Tatu mwaka 2013 ambayo inahusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu walengwa zaidi ya milioni moja katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,968 wananufaika na zaidi ya **shilingi bilioni 706** zimetumika.

Utekelezaji wa mpango huu umewezesha zaidi ya asilimia 95 ya watoto walio chini ya miaka 5 kutoka kaya za walengwa kuhudhuria kliniki, na zaidi ya asilimia 97 ya watoto wanaotoka kaya za walengwa kuhudhuria shuleni. Mahudhurio hayo kliniki na shuleni ni dalili njema ya kujenga nguvu kazi yenye afya bora na uelewa mzuri katika vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kutekelezwa kwa TASAF III jumla ya miradi 122 ya miundombinu yenye thamani ya **shilingi bilioni 4** inatekelezwa katika Halmashauri 13 za Mikoa ya Arusha na Njombe na tayari wawezeshaji katika ngazi ya Halmashauri na wajumbe wa kamati wamepatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa miradi katika maeneo yao.

Aidha, TASAF imekuwa ikizingatia matumizi ya Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli zake. Mifumo hiyo imekuwa ikiboreshwa katika awamu mbalimbali ili iweze kuongea na mifumo mingine ya kitaifa. Miongoni mwa mifumo hiyo ni Mfumo wa Kutambua na Kuandikisha Walengwa ambao ni dodoso la kielektroniki linalopokea taarifa kutoka ngazi ya jamii na kuzichakata ili kupata kaya zinazostahili kuandikishwa kwenye mpango wa kunufaika na ruzuku. Majaribio yameishafanyika katika Halmashauri za Siha, Mtwara Vijijini na Nanyamba Mji.

Mfumo mwingine ni Mfumo wa Malipo kwa Walengwa (e-payment system) ambao hutumika kuchakata malipo ya walengwa kwa kuandaa orodha ya malipo kwa ngazi zote zinazohusika na mwakilishi wa kaya. Mfumo huu unatekelezwa kwa majaribio katika maeneo ya utekelezaji kumi na sita (16) nchini ambapo **kaya 55, 350** zilikuwa zimelipwa kwa njia ya kielektroniki. Kupitia utaratibu huu malipo ya kaya hutumwa moja kwa moja kwenye akaunti aidha ya simu au benki ya mwakilishi wa kaya. Uzoefu umeonesha kwamba asilimia 95 ya wanaolipwa hutumia mitandao ya simu, na asilimia 5 tu ndiyo hutumia akaunti za benki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua hii na inashauri Serikali kuhakikisha mfumo unasambazwa na kutumika katika maeneo yote ya nchi kwa walengwa wa mpango, kwani una ufanisi na uwazi wa kutosha, malipo hufika kwa wakati na moja kwa moja kwa walengwa na hivyo kuokoa muda.

Ni ushauri wa kamati kwamba, Serikali ihakikishe inaondoa changamoto ya usajili wa line za simu ili kutokwamisha mfumo huu kutumika kwa walengwa wa ruzuku kwa kaya maskini. Ni wazi kwamba, iwapo walengwa wengi watahindwa kusajili line za simu kwa kukosa vitambulisho vya NIDA, mfumo huu hautaweza kutumika kwa kiasi kikubwa kama inavyotarajiwa.

Aidha, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kupata mkopo nafuu wa **shilingi triloni 1.035** (Dola za Marekani milioni 450) kwa ajili ya utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini katika awamu ya tatu ya TASAF (TASAF III) kwenye Halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar kuanzia mwaka 2019 hadi 2023.

Ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itahakikisha kuna usimamizi mzuri wa fedha hizi na kaya zote zenye sifa ambazo hazikuwa kwenye

mpango katika awamu zilizopita zitaingizwa kwenye mpango ili kila mwenye sifa aweze kunufaika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kutokana na Serikali kutochangia kikamilifu theluthi moja (1/3) kwa mujibu wa makubaliano na wadau wengine wa mpango huu.

Kwa mfano katika kipindi cha miaka sita na nusu ya bajeti kuanzia 2013/2014 – 2019/2020 (Januari, 2020) Serikali ilichangia **shilingi bilioni 8.11** tu kati ya **shilingi bilioni 70.01** zilizoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho sawa na takribani asilimia 11.58 tu ni kidogo sana. Mchanganuo zaidi wa uchangiaji wa Serikali umefafanuliwa zaidi kupitia jedwali **Na. 2** hapa chini.

**MCHANGO WA SERIKALI KATIKA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI  
MWAKA WA FEDHA 2013/2014 HADI 2019/2020 - JANUARI 2020**

Mwaka wa Fedha	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kiasi Kilichotolewa	Kiasi kilichobaki
2013/2014	18,500,000,000	3,000,000,000	15,500,000,000
2014/2015	14,000,000,000	0	14,000,000,000
2015/2016	14,000,000,000	600,000,000	13,400,000,000
2016/2017	14,000,000,000	0	14,000,000,000
2017/2018	3,000,000,000	750,000,000	2,250,000,000
2018/2019	3,000,000,000	3,000,000,000	0
2019/2020	3,514,206,000	757,102,800	2,757,103,200
<b>JUMLA</b>	<b>70,014,206,000</b>	<b>8,107,102,800</b>	<b>61,907,103,200</b>

**Jedwali Na. 02**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonesha kwamba, mpango wa kunusuru kaya maskini kwa takribani asilimia 89 umekuwa ukigharamiwa na fedha za mkopo na msaada kutoka kwa wahisani, jambo linaloleta wasiwasi kama unaweza kuendelea iwapo wahisani watajiondoa.

Kamati inaendelea kushauri juu ya Serikali kutathmini ushiriki wake katika mpango huu na kutoa mchango wake wa fedha kikamilifu ili kujenga utamaduni na kuandaa mazingira ya kugharamia mpango huu kwa fedha za ndani iwapo wahisani watajiondoa au watafikia ukomo katika kuchangia.



## f) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ulianzishwa kwa lengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Serikali iliamua kuuanganisha Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) na Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) Juni, 2019 jambo linaloufanya wakala kuwa sehemu ya Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

Miongoni mwa shughuli zilizokuwa zikitekelezwa na wakala ambazo sasa zitatekelezwa na TPSC ni pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali kwa njia ya midahalo na kwa njia ya Mtandao wa Video katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, Utawala Bora, Maadili, Afya na stadi za Utendaji ambazo zaidi ya washiriki 957 wamenufaika.

Aidha, kumekuwa na ushirikiano baina ya wakala na wadau wa ndani na nje katika kutoa huduma kutokana na mahitaji ya wadau. Wadau wapya ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu Huria (OUT) walijiunga ili kushirikiana na TaGLA na kupata elimu kuhusu manufaa ya kutumia tehamu na kufanya mikutano kwa njia mtandao wa video (video conference).

Wadau wengine ni pamoja na NIMRI, Shirika la Posta Tanzania, African Legal Support Facility (ALSF), DAWASA na Wizara ya Mawasiliano.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, hatua ya Serikali kuunganisha TaGLA na TPSC isihafifishe kazi zilizokuwa zikitekelezwa na wakala huo, badala yake kazi hizo ziboreshwe na kutekelezwa sambamba na

utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania.

**g) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika,** MKURABITA imekuwa ikiendelea kutekeleza mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Mpango huu umewezesha wananchi wanyonge kurasimisha mali ardhi na biashara na kuzigeuza kuwa nyenzo ya kupambana na kujikwamua dhidi ya umasikini.

Ili kufanikisha zoezi la urasilimishaji nchini, MKURABITA inawajengea uwezo watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara za kisekta kwa upande wa Zanzibar, kwa kuwapatia mafunzo ili waendeleze urasilimishaji katika maeneo yao.

Licha ya umuhimu wake, mpango huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ya maendeleo, na hata ile inayotengwa fedha zimekuwa zikitolewa kwa kiwango kisichoridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuanzisha mfuko endelevu wa Urasilimishaji katika Wilaya (District Revolving Fund) ili kuwezesha zoezi la urasilimishaji kujiendesha kupitia mfuko huo, ambapo imeweka **shilingi milioni 243** katika benki ya NMB kama dhamana ya mfuko huo. Aidha, tayari majaribio yanafanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Mji Njombe kwa Halmashauri hizo kukopa **shilingi milioni 100** kutoka mfuko huo kwa ajili ya urasilimishaji.

Hata hivyo, ni mtazamo wa Kamati kwamba kiasi kilichotengwa ni kidogo sana ikilinganishwa na halmashauri 185 zilizopo nchini ambazo urasilimishaji unahitajika.

Aidha, kumekuwa na changamoto kwa Halmashauri nyingi kutoona umuhimu wa zoezi la urasimishaji na hivyo kushindwa kutenga fedha za kuratibu zoezi hilo, na kutoshirikiana na waratibu wa MKURABITA. Takwimu zinaonesha hadi sasa ni Halmashauri 28 sawa na asilimia 15 ya halmashauri zote nchini (185) ambazo zimeweza kumiliki ajenda ya urasimishaji na kuweza kupima mashamba.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni ishara kwamba juhudi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha halmashauri zote nchini zinatambua umuhimu wa MKURABITA na kuweza kumiliki agenda ya urasimishaji ambayo utekelezaji wake utanufaisha wananchi na mamlaka za Serikali za mitaa kwa kuondoa migogoro ya umiliki wa ardhi, na kukuza uchumi wa wananchi ambao utasaidia kuongeza mapate ya Serikali.

**(h) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART).**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu ulianzishwa mwaka 2007 kwa Tangazo la Serikali Na. 120 ili kusimamia utekelezaji wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam kwa ufanisi na hivyo kupunguza msongamano ambao ni kero kubwa.

Mradi wa DART utatekelezwa kwa awamu sita na utahusisha barabara zenye urefu wa kilomita 146. Awamu ya kwanza ilikamilika na kuanza kutoa huduma Mei, 2016 kwa kutumia Mtoa Huduma wa Mpito "*interim service provider*" ambaye amekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uchache wa mabasi kwani aliingiza nchini mabasi 140 kati ya 305 yanayohitajika, na kukosa mfumo wa uhakika wa tiketi.

Serikali imechukua hatua kadhaa ili kukabili changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuanza mchakato wa kumpata Mtoa Huduma Kamili ifikapo Julai mwaka huu. Hatua hiyo itasaidia kuongeza mabasi na kuboresha huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, wataalam wa DART, TAMISEMI na eGA wanashirikiana kutengeneza mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kukusanya nauli ambao utakamilika Machi, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi hizo za Serikali. Hata hivyo, inapenda kushauri Serikali kuhakikisha DART inapata sheria mahususi, kwani kukosekana kwake kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala, ikiwa ni pamoja kukosa kanuni ambazo zingesaidia usimamizi na udhibiti wa matumizi mabaya ya miundombinu ya wakala.

**(i) Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo**

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki ambacho kilianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Na. 26 ya mwaka 1994 kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kushauri katika masuala mbalimbali yanayohusiana na uendeshaji wa Serikali za Mitaa.

Chuo kilianza kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada na kuanzia mwaka wa 2019/2020 kimeanzisha Shahada (Bachelor Degree) ya Utawala na Menejimenti katika Serikali za Mitaa. Aidha, chuo hiki kimekuwa kikiandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa kiasiasa na watendaji katika Serikali za Mitaa. Miongoni mwa viongozi hao ni Madiwani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ufanisi unaopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, chuo kimekuwa kikikabiliwa na changamoto kubwa ya ubovu wa barabara ya lhumwa – Hombolo (km 27) ambao unasababisha uharibifu wa vyombo vya usafiri na hivyo kusababisha gharama kubwa katika matengenezo. Aidha, kukosekana kwa uzio kuzunguka maeneo ya chuo kumekuwa kukisababisha wananchi wanaoishi maeneo ya jirani kuingia katika maeneo ya chuo jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa mali za chuo na wanafunzi.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, changamoto hizo zitatulwiwe ili kukiwezesha chuo kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kuwezesha Wanafunzi kusoma katika hali ya utulivu.

(j) **Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC)**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 36 ya Mwaka 1974 ili miongoni mwa mambo mengine, liweze kusimamia na kuendesha Soko Kuu pamoja na masoko mengine yatakayowekwa chini yake, kujenga masoko mengine katika Jiji la Dar es Salaam na kusimamia uendeshaji wake.

Shirika hilo ambalo lipo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI lina wanahisa wawili ambao ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Hisa asilimia 51) na Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali Kuu (Hisa asilimia 49), linamiliki mali zenye thamani ya **shilingi bilioni 56**. Aidha, mbali na Soko Kuu la Kariakoo Shirika lina maeneo mengine Tabata Bima na Mbezi Beach (Makonde).

Pamoja na shirika kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio, limekuwa likikabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja; na upungufu katika Sheria ya Shirika ambao unaathiri utendaji na uendeshaji, uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo kutokana na umri mkubwa (miaka 40), na zuiu la magari yanayoleta mazao katika Soko la Kariakoo kutokana na Sheria Ndogo za Manispaa ya Ilala na Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri changamoto hizi kufanyiwa kazi ili kuwezesha shirika hili kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kupata sheria bora ambayo itawezesha shirika kuwekeza vitega uchumi zaidi na hivyo kuongeza wigo wa mapato.

2.2.6 **Semina kwa Wajumbe wa Kamati**

(a) **Maadhimisho ya Mkataba wa Haki za Watoto na Vijana**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendesha na Shirika la Taifa la Watoto (UNICEF) kwa lengo la kuwakumbusha Wajumbe kuhusu haki za watoto. Semina ilisitiza kuhusu namna ambavyo kundi hili (watoto) muhimu katika jamii lina haki zinazopaswa kuzingatiwa na kulindwa na makundi mengine katika jamii.

Aidha, Wajumbe waliaswa kutumia nafasi yao ya uwakilishi na jukumu la kutunga sheria kuhakikisha wanaishawishi jamii kuhusu umuhimu wa kutambua, kuzingatia na kulinda haki za watoto. Miongoni mwa haki hizo ni kuishi, kupendwa, kusilikizwa, kupata huduma muhimu za elimu, afya na lishe.

Wajumbe wa Kamati walikumbushwa kwamba, iwapo watatekeleza kikamilifu jukumu la kutunga sheria kwa jicho la kumlinda mtoto ni wazi watasaidia kupunguza au kuondoa kabisa wimbi la watoto wa mitaani ambao huishi katika mazingira magumu, na hivyo kujenga vizazi bora kwa manufaa ya taifa letu.

#### **(b) Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) kwa ajili ya kuwajengea uelewa Wajumbe wa Kamati juu ya uongozi binafsi (personal leadership); pamoja na uongozi na wajibu wa kiongozi kwenye dola.

Semina ilieleza maana ya kiongozi, sifa za kiongozi bora na mwenendo ambao kiongozi anapaswa kuuonesha katika taasisi anayoiongoza na pia katika jamii inayomzunguka. Aidha, Wajumbe wa Kamati waliaswa kuepuka kujiingiza katika mwenendo na kutenda mambo ambayo yanaweza kuwashushia hadhi katika jamii.

Wajumbe walishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuweka utaratibu wa kisheria ambao utawezesha viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali na jamii, kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na taasisi ya Uongozi kabla ya kuanza kutumikia nyadhifa walizopewa.

## 2.2.7 Ziara za Ukaguzi wa Miradi

### **Utekelezaji wa Mradi wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project) katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Project*) unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia, katika Halmashauri za Majiji Matano (5) ya Mwanza, Tanga, Arusha, Mbeya na Dodoma; na katika halmashauri za manispaa tatu (3) ambazo ni Mtwara/Mikindani, Kigoma/Ujiji na Ilemela. Mradi una lenga kuimarisha na kuboresha huduma za msingi katika jamii ambazo ni pamoja na:-

- (a) Kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara, madampo ya kisasa, masoko, stendi za mabasi, vituo ya magari na mizigo, mifereji ya maji ya mvua, sehemu za mapumzikio na vizimba vya kuhifadhia taka; na
- (b) Kujenga uwezo wa taasisi katika kutoa huduma hususan katika kujenga misingi ya uchumi wa wananchi, kuwezesha utekelezaji wa uendelezaji wa mipango miji, kuimarisha ukusanyaji wa taka ngumu na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri.

Katika Jiji la Dodoma Mradi huu unatekeleza ujenzi wa soko la kisasa na stendi kuu ya mabasi katika eneo la Nzuguni; eneo la mapumzikio (recreational area) katika eneo la Chinangali, dampo la taka katika Kijiji cha Chidaya, kituo cha maegesho ya malori eneo la Nala na ujenzi wa kilomita 68.36 za barabara za lami. Miradi yote hiyo inakadiriwa kuwa na thamani ya takribani **shilingi bilioni 178.44**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi ya ujenzi wa stendi kuu ya mabasi na soko la kisasa katika eneo la Nzuguni ambayo utekelezaji wake ulikuwa katika hatua za mwisho kabla haijazinduliwa rasmi na kuanza kutoa huduma.

Mradi wa ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi unatekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 60, kwa gharama ya **shilingi bilioni 24.03**. Inatarajiwa kuwa stendi hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia mabasi 100 yanayoshusha na kupakia abiria kwa wakati mmoja, maegesho ya mabasi 150, magari binafsi 600 na taxi 250 kwa wakati mmoja, na jengo la abiria (waiting lounge) lenye uwezo wa kubeba abiria 6,000

kwa wakati mmoja watakaokuwa wamekaa. Aidha, kutakuwa na jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria 80 wenye hadhi maalum (VIP Lounge), vizimba vya biashara 60, migahawa na maduka kwa ajili ya kutoa huduma kwa abiria. Inaaminika stendi hii itakapokamilika itakuwa kubwa na ya kisasa kuliko stendi za mabasi zote katika eneo la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa soko la kisasa, mradi huu unatekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 27 kwa gharama ya **shilingi bilioni 14.65**. soko hili ambalo limepewa jina la **“Soko la Ndugai”** litakuwa na uwezo wa kuhudumia Wafanyabiashara 400 wa jumla na rejareja, kuegesha malori 30 wakati wa kupakia na kushusha mizigo kwa wakati mmoja, kuegesha magari mengine 600 kwa wakati mmoja, vizimba 172 vya biashara za bidhaa za mashambani, machinjio ya kisasa, maduka, na maeneo ya kupangisha wafanyabiashara wa bidhaa za viwandani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua madhubuti ambazo Serikali inazichukua ili kubadilisha sura ya Jiji la Dodoma kwa uboreshaji wa miundombinu. Hatua hiyo itarahisisha huduma za usafiri, uuzaji na ununuzi wa biadha na mifumo ya maji, na itaboresha madhari ya Jiji la Dodoma kwa kulifanya liwe na hadhi ya Mji Mkuu wa Serikali, na miongoni mwa majiji ya kisasa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

#### 2.2.8 **Muswada wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, ulileta Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019 (The e-Government Act, 2019) kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ili iweze kuufanyia kazi.

Muswada huu ulipendekeza kutungwa kwa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za Serikali Mtandao. Aidha, mamlaka hii itachukua nafasi ya iliyokuwa Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government Agency) ambayo ilianzishwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Na. 3 ya Mwaka 1977, Sura 245 na Kanuni zake.



Kamati ilitimiza wajibu wake wa kushughulikia Muswada huo kati ya Tarehe 21 hadi 26 Agosti, 2019 ambapo ilifanya uchambuzi wa kitaalam ulioboresha Muswada huo kwa kuzingatia maelezo na hoja zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, kuhusu vifungu vya Muswada, hoja za Wadau mbalimbali na kufanya tathmini na kuandaa maoni ambayo yalilisaidia Bunge kutunga Sheria ya Serikali Mtandao iliyokidhi viwango.

**Mheshimiwa Spika**, kutungwa kwa sheria hii kuliwezesha nchi yetu kuondokana na Wakala wa Serikali Mtandao ambayo ilitekeleza zaidi jukumu la ushauri badala ya usimamizi. Hivyo, kuwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ni kuwa na chombo cha kisheria ambacho kitahakikisha Sera, Sheria, Kanuni Viwango na miongozo kuhusu Serikali Mtandao vinazingatiwa kikamilifu katika taasisi za umma kwa lengo la kurahisisha matumizi ya Serikali Mtandao katika kuongeza ufanisi na ubora wa huduma za Serikali zinazotolewa kupitia mfumo huu.

Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha usalama wa Serikali Mtandao unazingatiwa kwa kiwango cha juu kwani ni eneo muhimu sana na iwapo litavamiwa linaweza kukwamisha shughuli zote za Serikali zinazotekelezwa kwa njia ya mtandao. Aidha, mamlaka iwezeshe kifedha na kiufundi ili iweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanayotokea duniani.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo: -

#### (a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

- i. Kiasi cha wa fedha kinachotengwa kwa TARURA ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inazozihudumia;
- ii. Mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambao TARURA inaupata kutoka Mfuko wa Barabara (RF) ni mdogo hivyo unapaswa kuongezwa;
- iii. Upungufu wa watumishi, uhaba wa ofisi na vitendea kazi unaathiri utendaji wa TARURA;
- iv. Iwapo Ukosefu wa sheria ndogo ndogo kwa lengo la kulinda na kuzuia uharibifu wa barabara zinazosimamiwa na TARURA kunachangia matumizi yasiyo sahihi ya barabara;
- v. Matumizi ya *force account* katika ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari nchini yanapunguza gharama na hivyo kuokoa fedha nyingi. Hata hivyo, ukarabati huo usiposimamiwa na wataalam (Wahandisi) unaweza kutekelezwa chini ya kiwango;
- vi. Utamaduni wa kukarabati majengo na miundombinu ya Shule za Sekondari na taasisi nyingine za Serikali utawezesha majengo na miundombinu hiyo kudumu kwa muda mrefu;
- vii. Miradi ya Soko la Kisasa, Stendi Kuu ya Mabasi, Kituo cha Mapumziko na Kituo cha Maegesho ya Malori inayotekelezwa kupitia Mpango wa Miji ya Kimkakati (TSCP), italeti tija na thamani halisi ya fedha "*value for money*" iwapo itasimamiwa vizuri na kuendeshwa kitaalam;

- viii. Kupatikana kwa Mtoa Huduma Kamili (*Service Provider*) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi inayohitajika kutasaidia kuboresha huduma ya usafiri kwa jiji la Dar es Salaam kupitia DART;
- ix. Kukosekana kwa Sheria mahususi ya DART kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wakala huo. Aidha, Wakala umekosa kanuni za kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu;
- x. Serikali itengeneze barabara ya lhumwa – Hombolo (km 27) kwa kiwango cha lami ili kupunguza uharibifu wa vyombo vya usafiri unaosababishwa na ubovu wa barabara hiyo;
- xi. Serikali iwezeshe chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo kujenga uzio ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya chuo kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani, na kuimarisha hali ya usalama;
- xii. Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo ni ya siku nyingi, ikifanyiwa marekebisho itasaidia kuondoa upungufu uliopo ambao unakwamisha shirika hilo kutekeleza majukumu yake na kujiendesha kwa tija; na
- xiii. Hatua ya Serikali kununua mashine za kukusanyia mapato za kielektroniki (POS) 7227 na kuzigawa kwa halmashauri zote nchini kutasaidia kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa mapato;

**(b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- (i) Hatua ya Serikali kuanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (*District Revolving Fund*) kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza urasimishaji itafanikiwa iwapo fedha za kutosha zitatolewa na kusimamiwa vizuri;
- (ii) Bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) inaathiri jitihada za kuongeza wigo ili kufikia maeneo mengi zaidi nchini;
- (iii) Hatua ya Halmashauri za wilaya chache (28) kumiliki ajenda ya urasimishaji inayotekelezwa na MKURABITA

inaonesha ni jinsi gani viongozi wa halmashauri nyingi nchini hawajaelewa vya kutosha umuhimu wa MKURABITA au hawana utashi wa kutekeleza mpango huo katika maeneo yao;

- (iv) Hatua ya Taasisi ya Uongozi kushirikiana na Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kuandika na kuchapisha vitabu vya wasifu (*autobiography*) wao, ni jambo la kupongezwa kwani litasaidia kuhamasisha viongozi wengine kujitokeza na kuandika vitabu. Aidha, utaratibu huo utasaidia kuweka kumbukumbu za viongozi hao kwa vizazi vijavyo;
- (v) Iwapo mfumo wa malipo wa kielektroniki (e-payment system) utatumiwa kikamilifu na TASAF kufanya malipo ya ruzuku kwa kaya maskini, utaongeza tija kutokana na uwazi na kuchukua muda mfupi;
- (vi) Hatua ya Serikali kutochangia kikamilifu katika mpango wa kunusuru kaya maskini kunafanya mpango kutegemea zaidi fedha za wahisani;
- (vii) Iwapo TASAF itafikia asilimia 30 ya vijiji, mitaa na shehia ambazo hazijafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini, itaondoa malalamiko kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo;
- (viii) Hatua ya Serikali kuhamishia iliyokuwa Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA) katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), ilenge kuboresha na kusambaza huduma za mafunzo kwa njia ya mtandao badala ya kuzihafifisha;
- (ix) Serikali iimarisha suala la usalama wa Serikali Mtandao ili kuzuia au kudhibiti uvamizi wowote unaoweza kukwamisha shughuli za Serikali zinazotekelezwa kwa njia ya mtandao; na
- (x) Serikali iiwezeshe kifedha na kiutaalam Mamlaka ya Serikali Mtandao ili iende sambamba na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano duniani.

## 3.2 Mapendekezo

### 3.2.1 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

**KWA KUWA**, TARURA inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi, ofisi na vitendea kazi vingine;

**NA KWA KUWA**; hali hiyo inaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya TARURA na hivyo kusababisha ishindwe kutekeleza kikamilifu matengenezo ya miundombinu ya barabara inazosisimamia;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali: -

- i. Kutenga bajeti ya kutosha na kutoa fedha kikamilifu ili kuiwezesha TARURA kutimiza majukumu yake kikamilifu ya kuhudumia mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inaousimamia nchini. Miongoni mwa njia za kuongeza fedha kwa TARURA ni kuongeza mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara (RF) kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 50. Aidha, Kamati iliyopewa jukumu la kupendekeza kuhusu jambo hilo ni vyema ikalikamilisha haraka ili kuruhusu utekelezaji; na
- ii. Kuendelea kuiwezesha TARURA kupata ofisi katika maeneo mbalimbali ya nchi, magari na vitendea kazi vingine pamoja na watumishi ili kupunguza uhaba uliopo

### 3.2.2 Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari

#### 3.2.2.1 Matumizi ya Force Account

**KWA KUWA**; matumizi ya *force account* katika ukarabati wa baadhi ya miundombinu na majengo ya Shule Kongwe za Sekondari nchini yameonesha mafanikio makubwa kwa kupunguza gharama na hivyo kuokoa fedha nyingi;

**NA KWA KUWA**, bado baadhi ya taasisi za umma hazijaona umuhimu wa kutumia utaratibu huu wa *force account* katika utekelezaji wa miradi yake na badala yake kuendelea kutumia kandarasi ambazo gharama yake ni kubwa;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha taasisi za umma zinatumia utaratibu wa *force account* katika utekelezaji wa miradi ili kuokoa fedha na kuzielekeza katika matumizi mengine. Aidha, Serikali ihakikishe kunakuwa na usimamizi wa kitaalamu katika miradi inayotekelezwa kwa *force account* ili kuhakikisha inazingatia viwango vya ubora vinavyotakiwa.

### 3.2.2.2 *Utamaduni wa kufanya ukarabati wa mara kwa mara*

**KWA KUWA**, ubovu na uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo ya shule kongwe za sekondari za Serikali vimesababishwa na kukosekana kwa utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo ya ubovu na uchakavu imesababisha Serikali kutumia fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo na ukarabati ili kurejesha miundombinu hiyo katika ubora unaotakiwa;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali na taasisi zake kujenga utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara katika miundombinu na majengo yake, ili kuepusha ubovu na uchakavu ambao ukarabati wake hugharimu fedha nyingi ambazo zingetekeleza shughuli nyingine.

### 3.2.3 **Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP)**

**KWA KUWA**, miradi ya vitega uchumi vya Soko la Kisasa, Stendi Kuu ya Mabasi, Kituo cha Mapumziko na Kituo cha Maegesho ya Malori, inayotekelezwa kupitia Mpango wa Miji ya Kimkakati (TSCP), katika Jiji la Dodoma imegharimu fedha nyingi ambazo ni mkopo;

**NA KWA KUWA**, miradi hiyo inahitaji kusimamiwa vizuri ili iwe na tija kwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa jamii, kuonesha thamani halisi ya fedha "*value for money*" na kuzalisha fedha ambazo zitachangia kulipo mkopo na kufanya maendeleo mengine;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha Uongozi wa Jiji la Dodoma unaendesha vitega uchumi hivyo kwa

ufanisi na faida kwa kuajiri na kuruhusu Mtaalam Mshauri atekeleze majukumu yake ya kitaalam kwa mujibu wa makubaliano bila kuingiliwa;

### 3.2.4 Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)

#### 3.2.4.1 Kukosekana kwa Mtoa Huduma Kamili

**KWA KUWA**, tangu Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam ulipoanza kutoa huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam Mei, 2016 umekuwa ukitumia Mtoa Huduma wa Mpito “Interim service provider”;

**NA KWA KUWA**, mtoa huduma huyo ameshindwa kutoa huduma kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na uchache wa mabasi (140 kati ya 305 yanayohitajika) aliyonayo, pamoja na kukosa mfumo madhubuti wa ukusanyaji nauli;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iharakishe mchakato wa kupatikana kwa Mtoa Huduma Kamili (*Service Provider*) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi inayohitajika ili aweze kuboresha huduma ya usafiri katika jiji la Dar es Salaam na hivyo kuwapunguzia wananchi adha ya msongamano wanayoipata;

#### 3.2.4.2 Kukosekana kwa Sheria mahususi ya DART

**KWA KUWA**, Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) hauna sheria mahususi ya kusimamia utendaji na utekelezaji wa majukumu yake;

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa sheria hiyo mahususi kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala, ikiwa ni pamoja na kukosa kanuni za kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu yake;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuiwezesha DART kupata sheria mahususi ambayo itasaidia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala. Aidha, sheria hiyo itawezesha kutungwa kwa Kanuni za DART ili kusimamia na kudhibiti uvamizi na matumizi mabaya ya miundombinu ya wakala.

### 3.2.5 Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo

#### 3.2.5.1 Ubovu wa barabara ya Ihumwa – Hombolo

**KWA KUWA**, barabara ya Ihumwa – Hombolo (kilomita 27) ni mbovu sana;

**NA KWA KUWA**, ubovu huo unasababisha uharibifu na uchakavu wa vyombo vya usafiri vya chuo na wafanyakazi wa chuo na hivyo kugharimu fedha nyingi katika matengenezo;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupunguza uharibifu wa vyombo vya usafiri unaosababishwa na ubovu wa barabara hiyo.

#### 3.2.5.2 Kukosekana kwa uzio kuzunguka eneo la chuo

**KWA KUWA**, hakuna uzio kuzunguka eneo la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaweza kuchangia maeneo ya chuo kuvamiwa na wananchi wanaoishi jirani na chuo na kuhatarisha usalama wa wanafunzi na mali za chuo na wanafunzi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukiwezesha chuo hicho kujenga uzio kuzunguka maeneo yake ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

#### 3.2.6 Upungufu katika Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo

**KWA KUWA**, Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo ni ya siku nyingi (tangu mwaka 1974) na hivyo kubainika kuwa na upungufu mwingi;

**NA KWA KUWA**, upungufu huo unaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo na kukwamisha uwekezaji wa vitega uchumi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuanza mchakato wa kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya



sheria hiyo ili kuliwezesha Shirika la Kariakoo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kujiendesha kwa tija kulingana na mazingira ya kisasa.

### 3.2.7 **Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

#### 3.2.7.1 **Kuanzishwa kwa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (District Revolving Fund)**

**KWA KUWA**, Serikali imeanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (*District Revolving Fund*) kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza urasimishaji kwa kuchangia ghama;

**NA KWA KUWA**, ufanisi wa utekelezaji wa mfuko huo utategemea fedha ambazo Serikali itaweka katika benki kama dhamana ya mikopo kwa halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kutekeleza zoezi la urasimishaji;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali ihakikishe inatenga na kutoa fedha za kutosha za dhamana ili kuwezesha Halmashauri nyingi kukopa katika mfuko huo na kutekeleza zoezi la urasimishaji kwa ufanisi;

#### 3.2.7.2 **Bajeti finyu inayotengwa na Serikali**

**KWA KUWA**, bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) inaathiri jitihada za kuongeza wigo ili kufikia maeneo mengi zaidi nchini;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha wananchi wa maeneo mengi kutofikiwa na MKURABITA na hivyo kukosa fursa ya kurasimisha ardhi na biashara zao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo ya MKURABITA ili kuwezesha zoezi la urasimishaji kuwafikia wananchi wengi na kuwapa fursa ya kurasimisha ardhi na biashara zao na kuzitumia kujikwamua kiuchumi.

### 3.2.7.3 Halmashauri chache kumiliki ajenda ya urasimishaji

**KWA KUWA**, Halmashauri 28 (sawa na asilimia 15) ndiyo zimepokea na kumiliki ajenda ya urasimishaji wa ardhi na biashara inayotekelezwa na MKURABITA;

**NA KWA KUWA**, hatua hiyo inaashiria ni jinsi gani viongozi wa halmashauri nyingi nchini ama hawajaelewa vya kutosha umuhimu wa MKURABITA au hawana utashi wa kutekeleza mpango huo katika maeneo yao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuweka mkakati wa makusudi wa kisheria utaohakikisha halmashauri zote nchini zinamiliki ajenda ya urasimishaji ili kuwezesha wananchi wa maeneo yao kutumia fursa hiyo kurasimisha ardhi na biashara zao na hivyo kujikwamua kiuchumi.

### 3.2.8 Usalama wa Serikali Mtandao

**KWA KUWA**, Serikali imeendelea kuhimiza na kujikita katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli zake na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao;

**NA KWA KUWA**, kutokana na umuhimu wake eneo hilo linaweza kuvamiwa na wadukuzi na wahalifu wa kimtandao na hivyo kuathiri au kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali, utoaji wa huduma kwa wananchi na pia upotevu wa raslimali fedha, taarifa muhimu na muda;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha inaimarisha usalama wa Serikali Mtandao ili kuzuia au kudhibiti uvamizi wowote unaoweza kukwamisha Serikali kutekeleza shughuli zake kwa njia ya mtandao pamoja na kuwahudumia wananchi.

Aidha, Serikali ihakikishe inaiwezesha kifedha na kiutaalam Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ili iende sambamba na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Duniani.

### 3.2.9 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

### 3.2.9.1 Mfumo wa malipo ya kielektroniki (e-payment)

**KWA KUWA**, TASAF imeanza majaribio ya malipo ya ruzuku kwa kaya maskini kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (e-paymanet) katika maeneo ya utekelezaji 16;

**NA KWA KUWA**, majaribio hayo yameonesha mafanikio makubwa kwa ufanisi, uwazi, malipo kufika kwa wakati na kwenda moja kwa moja kwa walengwa;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha TASAF inakamilisha maandalizi na kuanza kutumia mfumo huo kufanya malipo kwa walengwa wote wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini nchini.

### 3.2.9.2 Maeneo ambayo hayajafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini

**KWA KUWA**, asilimia 30 ya maeneo (vijiji/mitaa/shehia 5,693) nchini haikuingizwa kwenye awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inawanyima walengwa kati ya **355,000 – 426,000** wenye sifa katika maeneo hayo fursa ya kunufaika na mpango huo ili waweze kupunguza kiwango cha umaskini kutokana na shughuli za kiuchumi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali itumie kikamilifu mkopo wa riba nafuu wa **shilingi trilioni 1.035** ilioupata kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini na kuzifikia Halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar, na hivyo kuwapa wananchi wote wenye sifa fursa ya kunufaika.

### 3.2.9.3 Mchango wa Serikali katika Mpango wa kunusuru Kaya maskini

**KWA KUWA**, katika kipindi cha miaka sita na nusu ya bajeti kuanzia 2013/2014 hadi 2019/2020 (Januari 2020) Serikali iliweza kuchangia **shilingi bilioni 8.11** tu kati ya **shilingi bilioni 70.01** zilizoidhinishwa na Bunge;

**NA KWA KUWA,** kiasi hicho sawa na asilimia 11.58 ya fedha iliyoidhinishwa ni kidogo sana na hakifikii theluthi moja (1/3) inayopaswa kuchangiwa na Serikali na hivyo kuufanya mpango wa kunusuru kaya maskini kutegemea zaidi fedha za mkopo na msaada kutoka kwa wahisani;

**HIVYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuzingatia makubaliano ya uchangiaji katika mpango huo ambayo ni theluthi moja (1/3) kwa Serikali na 2/3 kwa wahisani.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, ninapohitimisha taarifa hii nikumbushe kidogo kuhusu dhana ya ugatuzi wa madaraka au upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization – D by D*) ambayo msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Utekelezaji wa dhana hiyo ya kikatiba kupitia sera iliyotungwa mwaka 1998 umesaidia kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi, na kuwashirikisha katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa manufaa yao.

Leo sote tu mashahidi kwa namna wananchi kwa kushirikiana na Serikali wanavyoshiriki katika shughuli za maendeleo kama ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, shule za msingi na sekondari, miradi ya maji, n.k kwa kuchangia nguvu zao na fedha.

**Mheshimiwa Spika**, ni kutokana na manthiki hiyo Kamati inashauri Serikali kuendelea kuunga mkono juhudi za Wananchi kwa kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilifu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi wanazozionesha katika kuchangia miradi ya kijamii na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. George Huruma Mkuchika, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI

Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) na Naibu Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Rais – TAMISEMI wakiongozwa na Mhandisi Joseph Nyamuhanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaru, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini mchango wao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu.

Iwapo wajumbe wasingejitoa kikamilifu na kwa weledi kushirikiana nasi viongozi wa kamati, ni hakika ufanisi usingepatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Kwa heshima kubwa ningetamani kuwataja majina yao, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,

5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
7. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
8. Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb
9. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mb
10. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb
11. Mhe. Venance Methusela Mwamoto, Mb
12. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
13. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
14. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
15. Mhe. Lusua Ursula Michael, Mb
16. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
17. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
19. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
20. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
21. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
22. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
23. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
24. Mhe. Mansoor Hilan Shaniff, Mb
25. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanaly Mohamedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote cha ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Pia, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili.

Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Modesta Kipiko, kwa

kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



Jasson S. Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA**

4 FEBRUARI, 2020